# *Kumwita Yesu Jukwaani*

Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, ndugu. Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

2 Baba wa Mbinguni, tuna furaha sana kwamba tungali tuko na Wewe, Bwana. Wakati vitu vingine vyote vimekwisha, tungali na Wewe. Wewe ni milele hata milele. Tunakushukuru Wewe, Bwana, kwa ajili ya mambo haya ya ajabu ambayo Wewe umetuonyesha katika wakati huu wa mwisho. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya uamsho huu na kwa ajili ya mahali hapa, kwa ajili ya Ndugu Carlson, kwa ajili ya ndugu wote wahudumu hapa karibu ambao wanajaribu kushikilia jambo lililo sahihi. Tunawaombea, Bwana, kwa moyo wetu wote, kwamba Wewe uta—Wewe utatupa uamsho mkubwa sana hapa Chicago, Bwana. Tujalie. Tunautazamia. Sasa samehe dhambi zetu na makosa. Na sasa, Bwana, mimi ni mchovu tukinena kimwili, lakini hata hivyo katika roho ninajisikia mwenye nguvu, nami naomba ya kwamba utatutia nguvu sisi sote sasa na kutuweka tayari kwa chochote Wewe ulicho nacho kwa ajili yetu usiku huu. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

3 Mwaweza kuketi. Hakika huu umekuwa ni wakati mkuu wa kuburudishwa kwangu. Nimeuthamini sana. Bwana Yesu ndiye tu anayejua jinsi ni—ninavyomshukuru Bwana kwa—kwa ajili ya yale Yeye ameninii . . . kwa yale Yeye ametufanyia.

4 Sasa ninataka kulishukuru kusanyiko hili kwa wema wenu wote na kwa ushirikiano wenu, kwa—kwa ajili ya kukaa karibu nasi na kulisikiliza Neno. Na hata hivyo, Jumapili usiku, baada ya kuwa na ibada ya Jumapili alasiri, mahali hapa pamejaa watu kabisa usiku wa leo tena. Tunashukuru sana kwa hilo.

5 Sasa ninataka kuwashukuru kwa ajili ya maskini ishara zenu za zawadi ambazo mmenitumia, kupitia Billy Paul. Katoni ya peremende na katoni ya biskuti ndogo, na, mwajua, katoni ya—ya viini vya walnati, na, loo, maskini tunu zote na kadhalika, zinamaanisha mengi sana kwa moyo wetu. Bila shaka tunathamini hilo. Kwa kawaida . . .

6 Nafikiri walisema walichukua sadaka ya upendo. Hiyo haikuwa ndiyo sababu ya mimi kuja, nyinyi nyote mwajua hilo, baada ya miaka hii yote. Lakini sadaka yoyote ya upendo, hata siiangalii, siioni. Inaenda moja kwa moja kwa—kwa . . . kwa ajili—kwa ajili ya ziara ya kimishenari nchi za ng'ambo, ambayo ninajiandaa kufanya mara moja.

7 Ninaingia ndani kuona baadhi yenu Wanorwe na Waswisi wazuri, makazi yenu asilia ambako mlitoka, huko Norwe na Swideni; na chini kuingia Denmark, kupanda hadi Finland.

8 Na kisha huko kumwona Ndugu Mattsson, huko Kenya na Tanganyika, kutembelea shule zake. Maskini ndugu huyo hakika amefanya kazi kwa bidii katika shule hizo. Ninaenda kumtembelea, kuiweka huduma ambayo Bwana Yesu amenipa, mbele ya hao vijana wa thamani kule ambao wanaondoka wakiibeba Injili.

9 Kutoka hapo, niendelee huko chini Afrika Kusini, nije, nikijaribu kurudi kupitia Uchina, Japani, na huko juu upande ule mwingine wa dunia.

10 Hivyo ndivyo tunvyofanya na hizi sadaka za upendo. Nasi ni. . .Kwa hiyo watu hawana uwezo wa kuidhamini mikutano, kwa hiyo mimi huendelea tu kuweka akiba kila kitu ambacho watu hunipa, kinachoingia. Hata sitoi pesa kwa cheki; inatiwa muhuri kutoka kanisani, na inaingia kwenye matoleo na inaweza tu kutumiwa kwa jambo hilo, ni hilo pekee, kwa hiyo basi ninajua haina budi kwenda sawa, mnaona, kwa hiyo tunashukuru.

11 Nami bila shaka nitafurahia, yapata asilimia themanini ya kusanyiko letu kote hapa Chicago kwa kawaida ni Wanorwe ama Waswidi, na—na wao kwa kweli ni watu wenye upendo.

12 Kusema kweli, ninaondoka Chicago, nielekee Tucson, Arizona. Huko ndiko ninakoishi sasa. Nami ninaishi. . . Aliyenipangisha nyumba ni maskini Mswidi. Ninaamini huenda ameketi hapa, usiku wa leo, Dada Larson. Ninaishi nyumbani kwake huko Tucson, Arizona. Sijamwona bado, bali anaishi hapa Chicago, na labda yuko hapa wakati huu endapo hayuko huko Tucson. Maskini mtu mpendwa sana, pamoja na mume mpendwa. Bila shaka tunamthamini.

13 Na sasa, Ndugu Carlson, Wafanyabiashara Wakristo, ndugu wote wahudumu kila mahali, Bwana awabariki sana. Bwana abariki mahali hapa na kupafanya mahali pakuu pa wokovu, ambapo, kimbilio ambako wenye haki wanakimbilia na kuwa salama. Hilo ndilo ombi langu nyenyekevu. Na nikiamini kwa moyo wangu wote ya kwamba. . .

14 Katika Jumbe hizi kali zinazokatakata, ikiwa nimejaribu kumwudhi mtu yeyote maksudi, Mungu anisamehe. Nisingefanya hivyo, kwa chochote kile. Lakini hata hivyo mimi ni mfungwa kwa hili Neno, mnaona, si—sina budi kudumu moja kwa moja na Hilo. Sisemi mambo magumu ku—kuwafanya watu wajisikie vibaya. Ninazungumza mambo vikali, wakati mwingine, kuwafanya watu waangalie, mnaona, mshangao, "Loo, angalia!" Mnaona, kuwafanya waliangalie, waone. Ndipo ukiwapata, labda wakati mwingine linawakasirisha. Na yapata mara tisa kwa kumi, kama wakichochewa kidogo, wataanza kuyachunguza Maandiko, ndipo Mungu anafanya yaliyosalia basi, mnaona. Hebu angalieni tu Maandiko. Kama nikipata kusema chochote ambacho ni kinyume na Maandiko,

unawajibika kuja na kuniambia juu yake, uniandikie, ama njia fulani kunifanya nijue. Na hiyo ndiyo sababu ninajisikia kuwajibika kwenu, kuyaeleza Maandiko. Si tu kujaribu kuyaeleza Hayo; ni kusema tu jinsi yalivyo. Hivyo ndivyo Hayo yasemavyo. Yaamini hayo, yaamini namna hiyo.

15 Sasa, kwa kweli ninathamini kuwatembelea. Nimekuja kwenu, mchovu. Nimekuwa tu nikifanya mahojiano na mikutano, na kadhalika, mpaka kidogo nikachoka. Na mikutano miwili kwa siku kidogo inakuwa, vema, niko tu kidogo mbali safarini kuliko nilivyozoea kuwa. Ndio kwanza tu nipite umri wa miaka ishirini na mitano, mwajua, mara ya pili. Hiyo ni kweli.

16 Vema, kuna jambo moja tu la kujutia, ya kwamba, sikumjua mapema maishani. Nilikuwa nikihubiri Injili nilipokuwa na yapata, nadhani, yapata umri wa miaka ishirini na miwili, na laiti ningalianza kuhubiri hapo nilipoweza kuzungumza, mvulana mdogo tu. Ni—ni—nilipoteza miaka hiyo yote ya thamani. Kwa mtu aliye kijana hapa, ninatumaini utachukua ambapo nilifanya kosa langu, kutoka kwenye yapata umri wa miaka kumi, kuendelea mpaka ishirini na moja ama ishirini na mbili, ninatumaini ya kwamba utaanza mapema, ili kwamba isikubidi kurejea kwa majuto ambayo ninarejea.

17 Bwana awe pamoja nanyi, ndilo ombi langu. Nami natumaini ya kwamba jambo fulani ambalo Bwana Yesu ameniruhusu kufanya, kwa karama . . .

18 Mnaona, mimi si ninii, nisingeweza kusema ni mhubiri, mnaona, kwa sababu mimi, kwanza, sina ufasaha wa kutosha, sina elimu. Hiyo ndiyo sababu nisingesema juu ya kuwa m—“mhubiri.” Kwa sababu, mtu anaposema, “mhudumu,” mara moja wanatarajia shahada ya chuoni, wanatarajia Daktari fulani mkuu wa Uungu, ama kitu fulani. Halafu basi unaposema “mhubiri,” kisha utumie maneno yangu, sarufi yangu mbovu, hiyo kidogo inaonekana kudhalilishwa.

19 Lakini Bwana alinituma kuwaombea watoto Wake wagonjwa. Basi mle ndani, kile ninachojua kumhusu Yeye, ninapenda kukieleza kwa moyo wangu wote. Kama nikifanya makosa, nyinyi niombeeni. Mimi si asiyeweza kukosea. Mimi ni ndugu yenu. Na sasa natumaini ya kwamba Mungu amefanya jambo fulani; kama hajafanya, naomba Yeye alifanye bado usiku wa leo, anene neno fulani ama kitu fulani ambacho kitawafanya kumwamini Yeye.

20 Mtu fulani alitaka kunipa zawadi hapa sio muda mrefu uliopita, ambayo, ilikuwa ni pesa nyingi kwelikweli. Nami nikasema, “Si—si—siwezi kuzichukua.” Nikasema, “Ni—nisingejua la kufanya nazo, unaona,” nikasema. Wao wakasema . . . Vema, vema, ilikuwa ni dola elfu moja, mnaona. Nami nikasema, “Nisingejua la kufanya nazo.”

21 Wakasema, "Vema, tunataka hizi ziwe za kibinafsi. Hatutaki hizi ziende kwa kanisa."

22 Haziendi kwa kanisa. Hii ni taasisi. Mnaona, zinaenda kwa kanisa, kwa jina la kanisa, bali ni hazina iliyowekwa kando kwa ajili ya nchi za ng'ambo pekee. Mnaona? Na kwa hiyo, hiyo, za—zawadi hazitozwi ushuru, kwa hiyo basi hazina budi kutumiwa kwa jambo hilo. Halmashauri ya wadhamini, wadhamini wameketi papa hapa usiku wa leo, wakinisikiliza. Na hiyo ni kweli. Nami nikasema . . .

Wakasema, "Tunataka hizi ziwe ni zako na familia yako."

23 Ilikuwa ni hundi. Nisingeweza kuichukua, mnaona. Nikasema, "Si—siwezi kufanya hivyo." Nikasema, "Hivi mnataka kunifanya kuwa na furaha?"

Kasema, "Hakika."

Nikasema, "Ninaweza kufanya nazo lolote nitakalo?"

"Naam."

24 Nikasema, "Basi acha nisaidie kulipia safari yangu ya nchi za ng'ambo." Tena nikasema, "Tunazo nguo za kutosha kuvaa. Watu hutupa nguo nyingi, pia tuna chakula mezani. Napata dola mia moja kwa juma kutoka kanisani." Ndipo nikasema basi, "Mimi, sisi, tunaendelea vema. Naomba nifanye nazo kile nitakacho." Na mimi . . .

Kasema, "Vema, ni zako, jifurahishe."

Basi nikasema, "Itanifurahisha sana."

25 [Ndugu mmoja anaenda mimbarani na kumkatiza Ndugu Branham, na anasema, "Hebu niseme tu neno moja. Kuna stesheni wagoni ya Oldsmobile ya samawati iliyoegeshwa moja kwa moja nyuma ya gari la Ndugu Branham. Sasa, watakapoondoka, watacheleweshwa mle ndani. Kwa hiyo kama upo hapa, naomba tafadhali uende na kulisogeza, stesheni wagoni ya Oldsmobile ya samawati kutoka Iowa. Sina nambari ya leseni yake, lakini labda unajua wewe ni nani, na unaombwa tafadhali kuliondoa gari lako. Asanteni,"—Mh.] (Naam, bwana.)

26 Upendo. Ha—hakika tunawathamini ninyi watu. Na sasa Bwana na awabariki sana. Na kama ukiwahi kupitia Jeffersonville, simama unione. Ukipitia Tucson, simama unione, na mimi—mimi nitafurahia kukuona.

27 Sasa daima, nikiishi Tucson, ofisi (kumbukeni) hubakia huko Jeffersonville. Billy Paul yuko moja kwa moja kule wakati wote, akijua mahali pa kuwasiliana nami wakati wowote. Mnaona? Atakuwa karibu ndiye mtu pekee atakayejua, kwa maana niko hudumani, kwanza mahali pamoja, pengine. Na huenda nikawa hapa, tuseme, Tucson; katika saa moja tangu wakati huo, Bwana amenipa ono, huenda nikawa njiani kwenda Hawaii, mnaona. Popote tu Yeye aniongozapo, huko ndiko

niendako, sio tu mahali pengine ila kuko huko, mnaona. Nanyi niombeeni. Kama sitawaona tena, upande huu wa mto, nitakutana nanyi ng'ambo Kule. Amina.

28 Sasa kabla ya kulikaribia Neno. Na, usiku wa leo, ninataka tu kuchukua da—dakika chache tu, kwa sababu nilikutana na baadhi ya marafiki zangu kule nje kutoka Jeffersonville, kisha nikakutana na kundi jingine la hao huko mtaani, nao wanakuja kwa motokaa usiku wa leo, baada ya ibada. Nami nilikuwa ninaenda kuhubiri juu ya somo la, *Kuhesabu Kinyumenyume*, huo ni wa urefu wa yapata saa mbili na nusu. Kwa hiyo wa—wasingefika Jeffersonville kabla ya mapambazuko asubuhi. Kwa hiyo, na wengi wenu enyi watu hamna budi kwenda kazini. Nanyi mmenisikia nikizungumza juma hili, na kufurahia kuwa pamoja nanyi. Na sasa usiku wa leo ninaenda kujaribu kufanya vizuri niwezavyo. Sasa, basi sitaninii, sitasema hivyo na sitasema lolote baya.

29 Sasa tunaenda kuomba kabla hatujalikaribia Neno.

30 Mungu mwenye rehema, nikitambua ya kwamba mimi ni . . . nimekuwa nikiwatazama watu hapa ambao labda baadhi yao sitawaona tena kamwe. Huu utakuwa wakati wetu wa mwisho kukutana. Kama ningerudi katika mwaka mmoja tangu sasa, wengi wangeninii, labda wengine watakuwa wameondoka, hata hivyo, watu wenye umri mkubwa. Na, Bwana, ninatambua ya kwamba kuna wengine hapa ndani usiku wa leo ambao ni wagonjwa, na kama Wewe hutagusa mwili wao kwa njia fulani, mimi . . . labda hawatakuwa hapa muda mrefu sana pia. Na tena, Bwana, huenda nisiwe hapa muda mrefu sana. Hatujui. Jalia tuwe waaminifu, basi, na wenye bidii, tukilikumbuka Neno la Bwana, kwamba, "Mambo yote yatatenda kazi kwa wema kwa wale wanaompenda Mungu."

31 Nami nitalisoma Neno, Bwana. Hilo tu ndilo ninaloweza kufanya ni kulisoma Neno, nasi tutakutegemea Wewe kusema jambo fulani ama kufanya jambo fulani litakalomwokoa kila mtu asiyeokoka hapa usiku wa leo. Jalia Neno la Mungu liwe halisi sana kwa baadhi ya watu, usiku wa leo, Bwana, ambao hawajaokoka, mpaka chini katika moyo wao watakukubali Wewe kama Mwokozi wao. Pia jalia Roho Mtakatifu aje miongoni mwetu, anene nasi, na kufanya kazi ya Mungu, kwa kuthibitisha Neno kwa ishara zinazofuata. Tujalie, Baba.

32 Na hapo maisha yatakapokwisha kabisa nasi tuje kwenye Uzima wa Milele, tutakuwa tu wenye shukrani kabisa, Bwana, mpaka wakati huo. Halafu kupitia wakati usio na mwisho, tunataka kuketi miguuni Pako, na kumtazama Yeye tunayempenda na Yule aliyetupenda. Mpaka wakati huo, tudumishe wenye afya na wenye furaha, tukikutumikia Wewe. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

33 [Ndugu fulani tena anakuja mimbarani na kuomba kwamba mwenyewe tafadhali aliondoe gari lake—Mh.]

34 Hebu tugeuke sasa katika Maandiko, kwenye mlango wa 4 wa Marko Mtakatifu, kifungu cha 35, kusoma, kama unapenda kufuatilia ama—ama labda kuliandika chini. Ninajua, watu wengi, wanachukua na kutia alama katika Bibla zao, fungu dogo, ambapo mhudumu anazungumzia, na kutoka hapo wa—wanapenda kulirejea. Nami ninapenda kusoma hizi Jumbe ndogo rahisi za Biblia na kuzizungumzia, linachangamsha tu moyo wangu kufanya hivyo. Kifungu cha 35 cha mlango wa 4 wa Marko Mtakatifu.

> *Siku ile kulipokuwa* jioni*, akawaambia, Na tuvuke mpaka ng'ambo.*
>
> *Wakauacha mkutano, wakamchukua vile vile alivyo katika chombo. Na vyombo vingine vilikuwako pamoja naye.*
>
> *Ikatokea dhoruba kuu ya upepo, mawimbi yakakipiga chombo hata kikaanza kujaa maji.*
>
> *Naye mwenyewe alikuwapo katika shetri,* akilala, kulala *juu ya mto; wakamwamsha, wakamwambia, Mwalimu, si kitu kwako kwamba tunaangamia?*
>
> *Akaamka, akaukemea upepo, akaiambia bahari, Nyamaza, utulie. Upepo ukakoma, kukawa shwari kuu.*
>
> *Akawaambia, Mbona* nyinyi *mmekuwa waoga? Imekuwaje hata hamna imani?*
>
> *Wakaingiwa na hofu kuu, wakaambiana, Ni nani huyu basi, hata* upepo *na bahari humtii?*

35 Kwa ajili ya mazungumzo ma—mafupi tu, usiku wa leo, ningependa kuchukua somo kutoka kwa hilo, na kuliita hivi: *Kumwita Yesu Jukwaani.* Hebu tumwite Yesu jukwaani.

36 Mwajua, ninaweza kuwazia jinsi Yeye alivyojisikia. Alikuwa ndiyo kwanza awe na siku nzuri sana. Na hiyo. . .Alikuwa amechoka. Na alikuwa akizungumza sehemu kubwa ya siku hiyo, akifundisha mifano. Kama utatambua, ya mbegu ya haradali na mambo mbalimbali. Alikuwa amekuwa na siku nzuri sana ya kuwaponya wagonjwa, na—na kufundisha, na nguvu Zake za kimwili zilikuwa karibu zimekwisha. Na kama mhudumu yeyote anajua, katika huduma zetu ndogo tu tulizo nazo, jinsi inavyotuchosha, kile hapana budi hicho kilimfanyia Yeye?

37 Kumbukeni, katika mwili Yeye alikuwa tu ni mwanadamu, bali katika Roho Yeye alikuwa ni Mungu. Lakini, mwanadamu katika mwili, hivyo basi mwili Wake ulikuwa ni mwanadamu ambaye alikuwa anaweza kupatwa na majaribu, anaweza kupatwa na maradhi, na sawa tu na yetu; kwa kuwa ilimbidi Yeye kuvaa, kuwa M—Mtu, mwanadamu. Halafu basi Yeye

alikuwa ni Mungu, katika Roho. Akasema, “Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Baba Yangu anaishi ndani Yangu.”

38 Wakati Yohana alipombatiza kwenye mto, Yordani, tunamwona Mungu akishuka kutoka Mbinguni kama hua, na Sauti ikisema, “Huyu ni Mwana Wangu mpendwa ambaye ndani yake ninapendezwa kukaa.” Sasa ukichukua ya asili, na kwa kweli jinsi imeandikwa, ni, “Ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake.” Mnaona? Lakini waliweka kitenzi kabla ya kielezi. “Ambaye ndani yake ninapendezwa kukaa, ama, Ambaye ndani yake ninapendezwa kukaa; Ambaye ninapendezwa kukaa ndani Yake.” Mnaona?

39 Yeye, Mungu, aliishi ndani ya Kristo, na ndani Yake mlikuwamo utimilifu wa Mungu, kwa jinsi ya mwili. Mungu akijidhihirisha Mwenyewe kupitia Yesu, na Yesu alikuwa ndiye thibitisho la Mungu. Mnaweza kulielewa sasa? Mnaona, si watu watatu; sifa tatu za Mungu mmoja. Si miungu watatu; miungu watatu, ukafiri. Mnaona? Si miungu watatu, sio. . .Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, sio miungu watatu mbalimbali. Ni Mungu mmoja katika madhihirisho matatu.

40 Mungu, Baba, katika umbo la Roho Mtakatifu alikuwa katika Nguzo ya Moto, na, Hiyo, hakuna mtu angaliweza kugusa karibu na Yeye. Alikuwa ni mtakatifu. Hakuna sadaka ya dhambi iliyotolewa; ni sadaka tu ya uwezekano.

41 Sasa, Nguzo ile ile ya Moto, ule Ubaba, ilishuka na ikafanyika Mungu katika Uwana. Yeye aliishi katika Nguzo ya Moto, hapa Yeye. . .katika Utukufu wa Shekina. Hapa Yeye aliishi katika mwili, ambao ulikuwa ni Mwana Wake ambaye Yeye alimuumba na kumfanya katika mfano wa mwanadamu, kwa hiyo hilo lilimfanya Mwana wa Mungu, Adamu wa Pili. Sasa, ilibidi Yeye aje kupitia tumbo la uzazi la mwanamke, si kama Adamu, kwa sababu hicho ndicho alichopaswa kuhukumu, kuzaliwa kwa mwanadamu kupitia mwanamke. Mnaona, kwa hiyo ilimbidi Yeye kuja kwa njia hiyo. Sasa huyo ni Mungu, Mwana, Mungu yeye yule. Na sasa Yeye, kwa kuutoa mwili huo bila dhambi, alifanya dhabihu ya mwanadamu.

42 Sasa, chembechembe, ama roho, uhai, hukaa katika damu. Na wakati seli ya damu ya mwana-kondoo ama mnyama ilipovunjwa, uhai uliokuwamo ndani ya seli hiyo usingeweza kurudi juu ya mwabuduo, maana alikuwa ni mnyama. Na sisi ni wanadamu, sisi ni tofauti. Mnyama hana nafsi. Mwanadamu ana nafsi. Kwa hiyo ro—ro—roho isingeweza kurudi juu yake akiisha kutoa dhabihu yake, bali hata hivyo aliitoa, na kwa unyofu, akinena kwa imani ya kwamba aliamini ya kwamba ile Dhabihu kamilifu ilikuwa inakuja.

43 Lakini wakati ile seli ya Damu ilipovunjwa, ndani ya Yesu Kristo, Mungu aliachiliwa. Mnaona, Yeye alikuwa ni Mungu. Hiyo Damu haikuwa ni ya Kiyahudi. Hiyo Damu

haikuwa ya Mataifa. Hiyo ilikuwa ni seli ya Damu ya uumbaji, Mungu Mwenyewe. Na sasa kupitia kwa hiyo Damu, ikifanya upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu, humsafisha mwaminio, inamwondolea mbali dhambi zake zote, kana kwamba kamwe hakuwa ametenda dhambi. Mungu huziweka katika Bahari ya Usahaulifu. Basi Mungu yeye yule aliyekuwa juu ya Yesu Kristo anaendelea ndani ya mwaminio, akifanya kazi zile zile ambazo Yeye alizifanya hapa, kwa kuwa Huyo ni Roho yeye yule.

44 Huyo hapo Mungu, mnaona, si miungu watatu. Loo, ni wangapi wenu ninyi wa utatu mlilichanganyisha hilo. Na jinsi ninyi watu wa Umoja mlilichanganyisha, pia, juu ya Yeye kuwa mmoja kama kidole chako. A-ha. Mnaona? Hao, wote wawili walilichanganyisha hilo. Mnaona? Hiyo ni kweli. Ati Yeye ni Mungu mmoja kama kidole chako, mmoja, angewezaje Yeye kuwa Baba Yake Mwenyewe? Mnaona? Mnaona, Yeye hawezi kuwa ni Baba Yake Mwenyewe. Na kama alikuwa na Baba mwingine nje ya Roho Mtakatifu, na kama Mungu ni mwanadamu, mtu, basi Yeye ni...Roho Mtakatifu alikuwa ndiye Baba Yake, na Mungu ni Baba Yake, Mathayo 1, kwa hiyo Yeye alikuwa ni Mwana haramu. Mnaona? Kwa hiyo huwezi kuifanya yoyote ya njia hizo mbili, wewe, zote mbili ni makosa.

45 Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika mwili wa Mwana Wake muumbaji. Mnaona? Sasa, hiyo ni kusema, Mungu alimuumba huyo Mwana.

46 Basi wakati ninyi watu wa Katoliki mnaposema, "uwana wa Milele," mnapata wapi neno kama hilo? Halina maana, kwangu mimi. Anawezaje Yeye kuwa wa Milele na awe mwana? Mwana ni kitu ambacho "kimezaliwa na," kinawezaje kuwa ni cha Milele? Milele kamwe haikuanza, kamwe haiishi, kwa hiyo ingewezaje kuwa ni uwana wa Milele? Loo, jamani!

47 Kama madhehebu haya hayajavuruga mambo, sijui ni kitu gani kimeyavuruga. Si ajabu watu hawawezi kuwa na imani, hawajui kitu cha kuamini. Hiyo ni kweli. Tunachohitaji ni kurudi kwa Biblia, kwa mtindo wa kale. Hiyo ni kweli. Kweli kabisa. Hiyo ni kweli.

48 Sasa, Yesu akiwa ni mwanadamu, kimwili, alikuwa amechoka, mchovu. Sasa amelala pale, amechoka; nguvu zilikuwa zimemtoka. Halafu Yeye akiwa ni Mungu, angeweza tu kufanya yale...

49 Sasa mnasema, "Angewezaje Yeye kuwa Mungu na awe mwanadamu?" Mnaona, hiyo hapo siri. Mnaona, katika mwili Yeye alikuwa ni mwanadamu, katika Roho Yeye alikuwa ni Mungu. Mnaona?

50 Mtu fulani aliniuliza, kasema, "Basi ni kwa njia gani, Yeye alimwomba Nani katika Bustani ya Gethsemane?"

51 Nikasema, "Nitakujibu hilo utakapolijibu hili: Je! unaamini una Roho Mtakatifu?"

"Naam."

52 Nikasema, "Basi unamwomba nani? Yeye huwa wapi wakati unapomwomba? Ambapo, unadai unaye Yeye, na hata hivyo unamwomba Yeye." Mnaona? Watu wananinii tu . . . wanapata tu wazo kidogo na kupotoka nalo, mnaona, hivyo ndivyo inavyoenenda.

53 Sasa, katika Roho, Yeye alikuwa ni Mungu. Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 3, mnaona, "Wakati, Mwana wa Adamu ambaye yuko Mbinguni sasa, hata hivyo amesimama hapa duniani, wakati Mwana wa Adamu ambaye sasa yuko Mbinguni." Ungewezaje kujibu hilo? Mnaona, Yeye alisema alikuwa Mbinguni wakati huo, na Yeye huyu hapa alikuwa amesimama duniani. Mnaona? Loo, jamani! Mnaona, kwamba, ilibidi awe ni Mungu, aliyepo kila mahali. Mnaona? Hakika, Yeye yuko kila mahali. Yeye anajua kila wazo. Kwa kuwa wa kujua yote, akijua mambo yote, Yeye anaweza kuwa kila mahali. Mnaona?

54 Kwa hiyo sasa tunamwona Yeye, akijua ya kwamba Yeye alikuwa na kazi kubwa mbele Zake, kesho yake, alikuwa anaenda huko Gadara. Na katika Gadara kulikuwako na mwendawazimu, mtu ambaye alikuwa amerukwa na akili, na alikuwa huko nje akiishi miongoni mwa pepo, na kujikatakata, maskini mtu ambaye asingeweza kuomba msaada wake mwenyewe. Na sasa tunaona ya kwamba Yeye yuko njiani Mwake huko. Ninaamini Yeye alijua yote juu yake. Baba alikuwa amemtuma Yeye kule. Alijua hilo.

55 Na sasa akiwa amechoka na ni mchovu, Yeye anarudi na kuchukua nafasi hii kwa ajili ya pumziko fupi wakati chombo kinapovuka bahari. Siku nzuri sana, labda yapata wakati huu jioni, ama baadaye kidogo, wanavuka bahari, sasa wakati Yesu alipoenda upande wa nyuma, nyuma katika shetri ya hicho chombo, labda aliingia kwenye chumba kidogo huko nyuma, na akalala juu ya mto. Na alipokuwa amelala pale, akipumzika, hao wanafunzi, waliwazia, "Sasa safari yetu ya siku imekwisha, ama kazi yetu kwa ajili Yake, sasa tunachukua jukumu letu la kawaida. Hebu tuanze tu kukivuta chombo."

56 Ni karibu kama tu wanafunzi leo hii, baada ya uamsho kwisha. Nasi sote tunajua umekwisha. Afadhali ulitatue hilo, umekwisha, ule uamsho mkuu ambao tumekuwa nao. Tunaokota tu masazo. Kwa hiyo, kwa kuwa umekwisha, kila mtu anaenda kwa kanisa lake mwenyewe na kadhalika, kuchukua, anairudia kazi yake ya zamani tena, chochote anachofanya.

57 Nasi tunaona walifanya hivyo wakati Yesu alipokuwa akipumzika kidogo. Na sasa hapana shaka walianza kushangilia juu ya kazi ambazo walikuwa wamemwona Yeye akifanya, na kujadiliana mmoja na mwingine. Loo, napenda kuliwazia hivyo,

kwamba—kwamba walikuwa wakishangilia juu ya uamsho waliokuwa wamekuwa nao siku hiyo.

58 Mwajua, ni kama tu wanafunzi Wake sasa. Mtakapoenda nyumbani, kama Bwana Yesu akikutana nasi usiku wa leo, na atafanya jambo la kipekee, kitu kama Yeye alichofanya jana usiku, kumfanya aliyepooza kusimama na kutembea, na mambo mbalimbali. Mnaona? Sasa, kama Yeye angefanya hivyo, ama mtu fulani apate kuokoka, ama kitu fulani, basi mtaenda nyumbani na labda, mama huyo na mume wake, watoto ama kadhalika, wataketi chini na kulizungumzia.

59 Hilo ndilo hawa wanafunzi, ninaamini, walikuwa wakifanya. Walikuwa wakizungumza kuhusu kile walichokuwa wameona kikifanywa. Loo, hapana shaka walikuwa wakifurahia hilo. Na hapana shaka walizungumzia matendo Yake, ya jinsi ambavyo Yeye alikuwa, alikuwa amejifanya Mwenyewe kuthitisha kwamba Yeye alikuwa ni Neno la Mungu lililoahidiwa. Sasa, Masihi, Yeye alikuwa amewathibitishia kwa matendo Yake, kwa Neno Lake, kwa matendo Yake, kwamba Yeye alikuwa Mtiwa mafuta. Sasa, neno "mtiwa mafuta," ama, ne—ne—neno *Kristo* linamaanisha "Mtu aliyetiwa mafuta." Kwa hiyo, kutakuwako na Mtu aliyepakwa mafuta juu ya manabii wote; kwa kuwa, manabii walikuwa na sehemu ya Mungu, bali Yeye alikuwa na utimilifu wa Mungu. Mnaona? Sasa, kwa hiyo mtu angeweza tu kuwa na sehemu. Yeye alikuwa na utimilifu wa Uungu, kwa jinsi ya mwili. Sasa walikuwa wakizungumza, na jinsi ambavyo hilo lilithibitisha kwamba Yeye alikuwa, kwa sababu kwa Neno walilokuwa wamejua kulihusu, na kumsikia Yeye akilielezea, liliwathibitishia kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Loo, ni mazungumzo makuu jinsi gani ambayo hapana shaka yalikuwa miongoni mwa hao wanafunzi!

60 Mmoja wao angesema, "Vema, basi, tunajua. Tumeridhika. Tunaamini Yeye ndiye yule Masihi." Sasa, unaona, walifikiri Yeye hakulielewa; Yeye alikuwa nyuma upande wa nyuma ya chombo. Kwa hiyo—kwa hiyo wakasema, "Hapana budi, tunajua ya kwamba Yeye hana budi kuwa mwanafunzi. . .hana budi kuwa ndiye Masihi aliyepakwa mafuta."

61 Kisha hapana shaka walijadili misimamo ya watu. Sasa hapana shaka walisema kitu kama hiki, "Kama tunaweza kuona hilo, hata hivyo sisi ni watu wasio na elimu, sisi wavua samaki kutoka kwenye ziwa hapa; na tunaweza kuona na kujua, na kusoma Maandiko yetu na kujua ya kwamba Yeye anatoshea ile picha kikamilifu, na tunajua kwamba Yeye ndiye aliyetambulishwa na Mungu, kwamba Yeye ndiye yule Masihi. Kwa nini wenye akili hawawezi kuliona? Wana shida gani, hata hawawezi kuliona?" Walizungumzia hayo maoni. "Baadhi yao, baadhi ya watu waliamini, wengine hawakuamini."

62 Mbona, ni sawa na ilivyo leo hii. Watu wengine

watamwamini Yeye leo, wengine hawamwamini. Lakini, Yeye, hilo halimbadilishi hata kidogo, Yeye angali ni yeye yule. Halimbadilishi Yeye.

63 Watu wengine katika siku hiyo, labda mazungumzo yao yalikuwa kitu kama hiki. "Mwajua, nilizungumza na kundi la watu huko chini leo, wakati sisi. . . Alipomgeuza yule samaki, akazidisha ile mikate na samaki. Nilikuwa nikizungumza na baadhi yao, nao wakasema, 'Huyo asingekuwa kitu chochote kingine ila Yehova, kwa kuwa Yehova Ndiye aliyeinyesha mikate kutoka mbinguni, kwa wana wa Israeli.' Nao wakasema, 'Hakuna mtu aliyewahi kuzungumza kama huyu. Mbona, Mtu huyu hana budi kuwa ndiye Masihi, kwa sababu tunajua Masihi ni Nabii. Na, lolote Yeye asemalo, Neno la Mungu liko pamoja na Yeye. Na lolote Yeye asemalo, halina budi kutimia. Basi Mtu huyu ndiye yule Masihi, kwa sababu, lolote Yeye asemalo, linatendeka.'" Amina! Ninapenda hilo.

64 Hiyo ndiyo sababu ninayo matumaini makubwa katika *Hili,* kwa sababu Hili ndilo Yeye alisema, nalo linaenda kutendeka. Hiyo ni kweli. Yeye, Yeye alisema. Hili ni Neno Lake. Lolote Yeye asemalo, litatendeka, "Mbingu zote na nchi zitapita bali Neno Langu halitapita."

65 Halafu basi wengine wao wakachukua upande wa kukana. Hao, wasioamini, wakasema, "Mtu huyu ni mpiga ramli tu. Sasa, Mtu huyu hawezi kufanya chochote. Tunajua ya kwamba Yeye ni m—mpiga ramli tu."

66 Sasa, walijua Yeye alikuwa na maisha ya kimwujiza, kwa kuwa Yeye angeangalia moja kwa moja ndani ya moyo wa watu na kuwaambia kile hasa walichokuwa wanafanya, kile walichokuwa wamefanya, kile kilichokuwa shida zao, na kile kingetukia. Na hilo halikushindwa kamwe. Lilitukia vivyo hivyo hasa. Na hiyo inaweza tu kuwa Mungu.

67 Sasa hakuna. . . mtabiri ama mpiga ramli anaweza kuja na kubahatisha kidogo na kukufanya nusu kitu fulani. Huyo ni ibilisi. Mtu yeyote anajua hilo. Kwa hiyo hukumwona mwaguzi au mpiga ramli huko nje akilidhihirisha Neno la Mungu, la hasha, hawafanyi hivyo. Wako kando mahali fulani wakichukua matoleo mahali fulani, ku—ku—kuwadanganya. Hiyo ni kweli. Nao wanaishi maisha ya namna yoyote.

Mtu huyu alithibitisha kwamba Yeye alikuwa ni Masihi.

68 Mnaona, roho hizo mbili zimekaribiana sana hata itawadanganya wateule kama yamkini. Lakini kama wameteuliwa, haitawadanganya. Mnaona? Lakini zinafanana sana, na hasa katika siku hizi za mwisho, Yesu aliahidi zitafanana, roho hizo mbili. Na jinsi hii, upande huo mwingine, huko mbali pande zote mbili hapa hata haifikiki.

69 Mahali vita vilipo, ni moja kwa moja huko juu pamoja na Shetani. Si mtu fulani ambaye huwabusu watoto wachanga, na—

na kuwazika wafu, na—na anabeba kisu cha mfukoni; bali mtu mwenye upanga wenye mikono miwili, moja kwa moja katika mstari wa mbele wa vita. Huyo ndiye, mnaona. Hilo ndilo jambo linalojalisha. Hapo ndipo ukali wa vita ulipo. Hapo ndipo adui anaposimama.

70 Na huko nyuma, vema, hawalioni. Mnaona, hampati shutuma yoyote. Hakuna kitu kinachokuja, ila tu, "Daktari *Fulani wa fulani*, hakika tuna furaha kukuona, kasisi wetu, ndugu, Baba Mtakatifu wa Kiungu Daktari *Nanii*." Mnaona? Loo, jamani!

Lakini unapokuwa huko juu, "Maskini huyo Beelizebuli, huyo ibilisi, huyo mnafiki, Yeye si kitu ila ibilisi." Inaanzisha mzozo kila wakati. Naam, bwana. Mnaona?

71 Hapo ndipo Yeye alipokuwa amesimama. Nao walijua kwa jambo hilo, hilo hapo hilo Neno lililothibitishwa, likathibitishwa kwamba ndilo.

72 Na kwa hiyo hilo, mnajua, huenda ilikuwa ni kijana Yohana ambaye moyo wa—wake haukuwa umetiwa makovu sana kwa theolojia chungu nzima, hapana shaka alisema kitu kama hiki, "Wazieni hilo! Papa hapa chomboni, Yuyu huyu ambaye ametambulishwa na Neno la Yehova, kuwa ni Mtumishi wa Yehova, Yule anayependezwa na Yeye, yuko moja kwa moja humu chomboni pamoja nasi. Ni hisi salama jinsi gani!"

73 Loo, laiti sisi usiku wa leo tungalipata tu hilo ono! Yehova yule yule, aliyeziumba mbingu na nchi, yumo mumu humu katika maskini chombo hiki chetu, wakati tukisafiri bahari adhimu ya maisha. Kwa kuwa, Roho Mtakatifu ni Yehova, katika umbo la roho, ndani yako. Unaona? Mungu, Roho Mtakatifu, ni Mungu Mwenyewe ndani yako. Yesu alisema, "Siku hiyo mtajua ya kwamba Mimi ni ndani ya Baba, Baba ndani Yangu, Mimi ndani. . .nanyi ndani Yangu." Loo!, Loo, jamani!

74 Ndipo Mungu, yote aliyokuwa Mungu, Yeye aliyamimina ndani ya Yesu; na yote aliyokuwa Yesu, Yeye aliyamimina ndani ya Kanisa Lake, akajigawa Mwenyewe kwenye Siku ya Pentekoste. Ile Nguzo ya Moto ilishuka chini ikajipasua Yenyewe, ule Utukufu wa Shekina, na kuitia Hiyo ndani ya watu mbalimbali. Ndimi za Moto zilionekana juu ya kila mmoja; Roho Mtakatifu, Mungu, akijitambulisha Mwenyewe katika wanadamu. Amina.

75 Nena kuhusu neema ya ajabu, jinsi inavyosikika tamu? Ni salama jinsi gani ilivyo! Jinsi tunavyojisikia salama, kujua ya kwamba tunapoendesha motokaa kwenye barabara kuu, chochote tunachofanya, kwamba Yesu amelala ndani ya chombo. Amina. Yule Ambaye anaweza kufanya mwujiza wowote, anaweza kufanya chochote Yeye anachotaka kifanywe, kukifanya tena, ajitambulishe Mwenyewe kikamilifu. Yeye yuko ndani ya chombo chetu tunaposafiri katika bahari hii

kuu ya maisha. Sawa na vile Yeye alivyokuwa wakati huo, ndivyo Yeye alivyo sasa. Ni hisi ya jinsi gani ya usalama, tunaposafiri maji yaliyotibuliwa ya maisha. Wakati huyu Mel Johnson, yule mwimbaji hodari, maskini uimbaji wa Kiswisi, "Wakati nimeshavuka mto Yordani." Wazia tu, wakati unapofika pale chini mtoni, Yeye atakuwapo. "Sitawaacha wala kuwapungukia." Ni ahadi jinsi gani, tukisafiri maji haya yaliyotibuliwa.

76 Walikuwa ni kitu kama sisi leo hii, hao wanafunzi huko nje kwenye chombo hicho usiku huo, baada ya ule uamsho, walikuwa wakisherehekea matokeo yake.

77 Sasa labda katikati ya miamsho sasa, tunatafuta mchocheo mwingine, ambapo hapana budi jambo fulani litukie sasa litakalolikusanya Kanisa pamoja. Itabidi kuwe na mgandamizo wa namna fulani. Mungu daima hulifanya namna hiyo, kuwakusanya watu Wake pamoja. Ninaamini ya kwamba tayari unafanyizwa, ambao utafungia nje kila kitu ambacho hakitakubaliana nao, ndipo basi unaenda kuleta Kanisa pamoja upesi. Nasi tunangojea jambo hilo kutendeka, na sisi tunaishi kwenye matokeo ya uamsho mkubwa ambao ndio kwanza tumalize, na Yeye anapumzika.

78 Yeye alikuwa akipumzika wakati huo kama vile Yeye alivyofanya wakati alipoimaliza kazi Yake katika Mwanzo. Biblia ilisema, "Na siku ya saba, Mungu alipumzika kutokana na kazi Zake zote." Na sasa Yesu alikuwa amemaliza siku hiyo, na Yeye alikuwa anapumzika kutokana na kazi ambazo Yeye alikuwa amefanya siku hiyo, akipumzika kwa ajili ya kazi ku—kuu itakayoanza kesho. Mnaona, akipumzika kidogo.

79 Na hivyo ndivyo ninafikiri Yeye anafanya sasa. Uamsho hauko miongoni mwa watu. Huwezi kuona ile shauku ya awali. Tulikuwa na, yapata miaka kumi au kumi na mitano iliyopita wakati uamsho ulipoanza, mmoja wa miamsho iliyodumu muda mrefu kuliko yote tuliyopata kuwa nayo. Na historia inaonyesha tu uamsho hudumu si zaidi ya miaka mitatu, kama ni mingi sana. Nasi tulikuwa na mmoja katika siku hii ya mwisho sasa, kwa yapata miaka kumi na mitano, ambapo mioto ya uamsho iliwaka kote u—ulimwenguni.

80 Lakini sasa inaonekana unatulia. Tunashangaa, kila mtumishi aliyejazwa na Roho, na kutazama juu, "Bwana Yesu, ninajua ya kwamba jambo fulani linaenda kutukia. Ninahisi msukumo ukija. Ninakupenda Wewe, Bwana. Na sasa na—nataka kukuona Wewe katika amani, Bwana. Tusaidie. Tunakungojea Wewe." Hivyo karibu ndivyo jinsi maoni yalivyo.

81 Hivyo ndivyo, hao wanafunzi wakizungumzia kile walichokuwa wameona, na ndipo, mara ghafla, shida ikatokea.

82 Huyo ni Shetani. Hatawaacha kupumzika juu yake muda mrefu sana. Mnapoanza kuzungumza juu ya Bwana Yesu, na kuhusu kazi Zake, yeye atakuwa papo hapo kukatiza hilo.

83 Ndipo shida ikainuka, kwa ghafla. Chombo kikaanza kuyumbayumba, matanga yakapasuka, makasia yakavunjika, ndipo maji yakajaa chomboni. Shida imekuja! Unaona, ilitukia ghafla. Matumaini yote ya kunusurika yalikuwa yamekwisha. Ingawa walikuwa wamemwona Yeye akifanya mambo mengi sana makuu; shida inapoingia, wanasahau yote kuhusu hayo.

84 Sasa ninataka kuwaulizeni jambo fulani, kama ndugu. Huo karibu si ndio mwelekeo wa watu leo hii? Tutakuja kanisani hapa, na kupaza sauti na kumsifu Mungu, wakati ndugu zetu na kadhalika, wanapolinena Neno, nasi tunaweza kusikia hizo ahadi. Tunamshukuru tu Mungu kwa yale aliyofanya, tunasikiliza ushuhuda wa mtu huyo akisema, "Wakati mmoja nilikuwa kipofu, macho yangu yalikuwa mapofu, sasa ninaona." Mmoja anasema, "Daktari alikuwa amenikatia tamaa, kwa kansa, na katika majuma mawili, ama siku mbili, ama chochote kile, hapakuwapo na chembe moja ya kansa. Hiyo imekuwa ni muda mrefu uliopita. Hawawezi kuipata tena hata hivyo." "Nililala, nikiwa nimefungwa kwenye kiti cha magurudumu, nimepooza; ninatembea vizuri kama mtu mwingine yeyote." Tunazisikia shuhuda hizo.

85 Lakini kama tu hilo, acha ipige maskini nyumba yetu wakati mmoja, ndipo tunasahau yote kuhusu utukufu huo ambao tumekuwa tukifurahia, mambo hayo yote makuu; loo, ni sisi sasa. Mnaona, mambo hayo hufanyika kwa kusudi fulani, yanafanyika yapate kukujaribu. Sasa, shida ambayo hatuwezi kutatua, inaonekana kama madaktari hawawezi kutatua, wala hakuna kinachoweza kuitatua.

86 Walijaribu kuyavuta makasia yao; yakapasuka. Walijaribu matanga yao; yakavunjika. Wakakimbilia katikati ya chombo; kikajaa maji. Mnaona, Shetani alidhamiria kuwaangamiza. Sasa alifikiri alikuwa amempa Yesu usingizi, mbali na hao, na ndipo angeweza kuwanyemelea.

87 Sasa hivyo ndivyo ilivyo leo hii. Shetani anapopata nafasi, huyu hapa anakuja. Mnaona? Nawe unamwendea daktari, anasema, "Hakuna kitu unachoweza kufanya; umeenea. Nani? Hatuna kitu kwa ajili ya ugonjwa wa akili. Hatuna kitu kwa ajili ya magonjwa ya akili. La, hatuwezi kufanya chochote. Baridi yabisi? La, hatuwezi kufanya chochote kwa hiyo. Labda tunaweza kukupa kortisoni, na hiyo itakuua, kwa hiyo hatuna chochote kwa ajili yake. Lukemia? Hatuna kitu tunachoweza kufanya kuihusu." Mnaona, ndipo unapata shida zote.

88 Lakini, angalia nyuma, hivi Yeye hajaponya lukemia? Hivi Yeye hajaponya kansa? Hivi Yeye hajafanya kila kitu sawa? Hivi Yeye hajalitimiza Neno Lake? Mnaona, tunahangaika

wakati inapopiga maskini chombo chetu. Maskini ganda hili tunalosafiria ni nyonge, hata hivyo, hujazwa na mashaka, ulimwengu.

89 Angalieni, shida wasiyoweza kutatua, ndipo hofu inaingia, kama tu ilivyo sasa. Hata tuna hofu katika matatizo ya kitaifa. Tuna hofu katika matatizo kanisani. Tuna hofu kotekote, kila mahali. Sasa tunasema, "Vema, sasa, tunaweza kufanya nini juu yake?" Laiti tungaliweza tu kukumbuka ya kwamba Yeye yumo ndani ya chombo. Mnaona? Mnasema, "Lakini ni..." Naam. "Je! Yeye yumo chomboni?"

90 Hapa, *Huyu* Ndiye, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Nalo Neno ni "yeye yule jana, leo, na hata milele." Ingali bado ni kwamba uchukue tu *Hili*! Ndilo suluhisho. Ndilo dawa. Ndilo tiba kwa kila kuchanganyikiwa. Ndilo—ndilo tiba kwa kila kansa. Ndilo tiba kwa kila maradhi. Ni Mungu akidhihirishwa katika Neno. "Neno ni Mungu." Yesu alisema, "Ni mbegu." Mbegu ikipandwa katika aina ya udongo unaofaa, itakua kile hasa ilicho, na kila ahadi itazalishwa. Tunasahau yote kulihusu, kujua kwamba Yeye yumo chomboni.

91 Walipaswa kujua ya kwamba Yeye alijua jambo hilo lilikuwa linaenda kutukia. Mnaamini hilo? Hakika, Yeye alijua hilo. Yeye alijua, wakati wote, lilikuwa linaenda kutendeka. Kwa nini? Alifanya hivyo tu kuthibitisha, kuijaribu imani yao.

92 Na wakati mwingine Yeye hufanya jambo lile lile kwa ajili yangu na yako, Yeye huacha mambo yatukie kusudi tu aone kile tutakachofanya kuyahusu. Mnaamini hilo? Maandiko yalisema kwamba, "Kila mwana amjiaye Mungu hana budi kujaribiwa, kurudiwa, kuthibitishwa." Shetani atakufanya uthibitishe kila inchi ya ardhi unayodai; hakika atakufanya. Kwa hiyo, wakati mwingine Mungu huacha mambo hayo yatukie.

93 Sasa, kumbukeni, wote walikuwa wanataharuki. Matumaini yote yalikuwa yamekwisha. Chombo chao kilikuwa...Matanga yao, yale waliyokuwa wamezoea kusafiri kwayo, yaliangamia. Makasia, ambayo walikuwa—walikuwa wamevuta kwake, yalivunjika. Mawimbi yalikuwa yamekivuruga na kukiinamisha kile chombo upande mmoja, na kadhalika. Matumaini yote yalikuwa yamekwisha. Na hata hivyo, moja kwa moja pamoja nao, akiwa amelala chomboni, alikuwa Mmoja Ambaye alikuwa amethibitisha Yeye alikuwa ndiye Muumba wa mbingu na nchi. Amina. Alikuwa amethibitisha kile Yeye alichokuwa, kwa ishara na maajabu, kwamba Mungu alikuwa amelichukua Neno Lake ambalo Yeye alisema Masihi Wake angefanya, na alikuwa amemthibitisha Mtu huyo kuwa ni Masihi Wake. Na Yeye alikuwa amelala tu nyuma ya chombo, kutoka kwao, na hata hivyo waliogopa sana.

94 Utukufu! Ninajihisi kama...kile mnachowazia niko, mtakatifu anayejibingirisha. Vema, sasa angalieni wakati... Ninajua hilo halisikiki sana kama kasisi, lakini li—linanifanya nijisikie vizuri kulisema, haidhuru. Mnaona?

95 Kwa hiyo angalia hapo, msaada wao—wao ulikuwa umekaa pale pale, nao walikuwa wamesahau yote kuhusu Huo. Yesu alikuwa amethibitisha kuwa Mungu yule hasa aliyeweza kuumba mkate, siku moja kabla ya hapo, siku hiyo hiyo, kuumba samaki. Alithibitisha kwamba Yeye alikuwa ndiye Muumba, nao walikuwa bado wanashangaa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

96 Yesu alisema, "Kama—kama siyafanyi mambo hayo yaliyoandikwa juu Yangu, basi msiniamini Mimi; bali nikifanya mambo hayo yaliyoandikwa juu Yangu, yanashuhudia na kuwaambia kuwa Mimi ni nani." Loo, jamani!

97 Kama ukidai kuwa Mkristo, Biblia hapa inakwambia kile Mkristo anapaswa kuwa. Marko 16 itakwambia kama wewe ni mwaminio, au sivyo, unaona, inakwambia kile unachopaswa kuwa.

98 Yesu alisema, "Ni nani kati yenu anayeweza kunihukumu Mimi kwamba nina dhambi?" Dhambi ni kutokuamini. "Kama sijathibitisha hasa kabisa, kwenu, kile ninachopaswa kuwa."

99 Mjumbe yeyote mkuu kama huyo ametabiriwa kwetu katika Biblia. Daima tunaweza kupata mahali pake katika Maandiko. Hiyo ndiyo sababu Roho Mtakatifu leo hii ametabiriwa kwetu katika Biblia, nasi tunajua ya kwamba Yeye yupo hapa. Nasi tunajua kwa Maandiko, thibitisho la kile Yeye alicho. Tuliona jinsi Huyo alivyofanya hapo mwanzo, tumeona jinsi Huyo alivyofanya katika Kristo, tunaona jinsi Huyo anavyofanya leo hii. Mnaona, tunajua Huyo ni Roho Mtakatifu, ama siye, kwa sababu Huyo hudhihirisha na kulithibitisha Neno la Mungu, hulifanya Hilo kuwa hai.

100 Sasa, "Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Yachunguzeni Maandiko, Hayo yanawaambia kwamba Mimi ni Nani." Walipaswa wawe wamejua jambo hilo, Yeye alikuwa ni Mungu yeye yule ambaye angeweza kuumba mkate, Yeye pia aliziumba pepo na mawimbi. Hakika. Yeye si tu sehemu ya Mungu; Yeye wote ni Mungu. Yeye aliziumba pepo na mawimbi. Kama—kama ilibidi vitu vingine vimtii Yeye, na Yeye alikuwa ndiye Muumba, hivi pepo na mawimbi hazikupaswa kumtii Yeye pia? Amina.

101 Angalieni, hebu tukumbuke, Yeye pia aliiumba miili yetu. Na hivi miili yetu haitabidi imtii Yeye? Amina. Wewe salimisha mawazo yako Kwake, salimisha maisha yako Kwake, salimisha imani yako Kwake, kisha uone huo mwili ukitii yale Yeye asemayo. Kama wewe ni mlevi na huwezi—huwezi kuacha kunywa pombe, yasalimishe maisha hayo Kwake na, tazama, hutakunywa pombe tena. Kama wewe ni mvuta sigara mzoefu,

na ulijaribu kuziacha wala huwezi kuziacha, salimisha tu hizo Kwake na uone kinachotukia. Ataufanya mwili huo urudi kwenye utii wa Neno. Naam, bwana. Lakini huna budi kuusalimisha Kwake. Huna budi kumwamini Yeye. Yeye aliumba miili yetu; inatii mapenzi Yake pia. Mnaamini hilo? Kama wewe ni Mkristo, inakubudi kuamini.

102 Unasema, "Ati Yeye huifanya miili yetu kutii? Loo, ninaamini tuna mamlaka juu ya hiyo." Basi huja—hujajisalimisha kikamilifu.

103 Kwa kuwa, wewe si mali yako mwenyewe; umekufa. "Wewe mwenyewe umekufa, na maisha yako yamefichwa katika Mungu kupitia Kristo, na kutiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu." Utayaondokeaje hayo? Nafikiri tunahitaji uamsho. "Uhai wetu umekufa." Tumekufa; mawazo yako mwenyewe. Unawaza mawazo safi. Yale mawazo ya kale ya kilimwengu yanayokupotosha, umeyafia hayo. "Na maisha yako yamefichwa katika Mungu kupitia Kristo, na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu." Ni mahali pa jinsi gani! Ni usalama jinsi gani! Loo, jamani! Muda gani, hata uamsho unaofuata? "Mpaka siku ya ukombozi wenu." Waefeso 4:30, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwaye mmetiwa muhuri hata siku ya ukombozi wenu." Ni hisi ya usalama jinsi gani, kujua na kumwona Roho Mtakatifu akibadilisha tabia yako kutoka kwa mtu mwovu. Amina. Ndipo tunajua tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani, tunamwona Roho Mtakatifu akiishi ndani yetu, Maisha Yake.

104 Paulo alisema, "Maisha niliyoishi wakati mmoja, siyaishi tena. Loo, sio mimi, bali Kristo aishiye ndani yangu!" Haya basi, alikuwa amepita toka mautini kuingia Uzimani, Naye Kristo alikuwa hai ndani yake. Salama salimini! Kristo Ndiye aliyekuwa akikiongoza kile chombo; ilimbidi Paulo kuketi tu kimya na kumtii Yeye.

105 Tazama, Mungu ataifanya miili yetu imtii sana, hata Yeye alisema katika Yohana Mtakatifu mlango wa 6, "Yeye aulaye mwili Wangu, na kunywa Damu Yangu, yuna Uzima wa milele, nami nitamfufua kwenye siku ya mwisho." Liwazie, miili yetu hutii wakati hatuna mamlaka juu yake tena, nayo inageuka kuwa kijiko kimoja cha mavumbi, Mungu ataunenea mwili huo nao utafufuka tena katika mfano wa Yesu Kristo aliyefufuka. Unafadhaika nini kuhusu *huu*? Kama uko mikononi mwa Mungu, uachilie, amina, kwa maana Yeyeataufufua, siku ya mwisho. Aliahidi kufanya hivyo, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Imeadikwa katika Neno Lake. Unaogopa nini kuhusu hili basi, maskini chombo hiki cha kale? Yeye yuko ndani yake.

106 Kama Yeye hayuko ndani, usiondoke usiku wa leo mpaka Yeye aingie ndani. Ni jambo la hatari kujaribu kusafiri bila Yeye. Utazama, hakika.

107 Lakini huwezi kuzama. Ukizama, Yeye atakuinua tena, kwa hiyo inaleta tofauti gani? Uzima wa Milele, Mungu anayeweza kufanya maumbile yote kumtii Yeye. Loo, ninaupenda ule wimbo wa kale wa kanisa:

> Pepo na mawimbi zinatii mapenzi Yake.
> "Amani, tulia! Amani, tulia!"

108 Kila kitu hakina budi kumtii Yeye. Maumbile yote hayana budi kumtii Yeye. Yeye ndiye Muumba wa maumbile. Amina.

109 Baada ya wanafunzi kujikuta hawana la kufanya, hapana shaka ilifunuka kwao. Baada ya wao kuona wasingeweza kufanya lolote juu yake, hapana shaka iliwafunukia, "Aisee, tuko katika hali mbaya sana hapa! Loo, ninaenda kufa. Sitaki kuzama. Hii . . . "

110 Mmoja wao hapana shaka alisema, "Ngoja kidogo, ngoja kidogo! Hivi iliwahi kukufunukia, ya kwamba Yeye amelala papo hapo? Hapa tumekuwa tukizungumza yote juu Yake, tukishuhudia habari Zake, kuhusu zile kazi kuu, na kumdai Yeye kuwa Masihi, naye Huyu papa hapa pamoja nasi." Loo! Loo! Utukufu! Loo, ni hisi ya jinsi gani!

111 Hivi uliwahi kufikiria kwamba ulikuwa umefika mwisho wa barabara? Yapata miezi minane iliyopita nilipoona ono nikiwa nyumbani, nanyi mnajua kuhusu hilo, *Mabwana, Ni Wakati Gani?* Nilipoona hilo, nikasikia ule mlipuko ukilipuka kwenye ono, nikawaona Malaika saba wakija, wakaninyakua. Niliwaambia ninyi nyote, "Huenda ikawa huu ndio mwisho wa safari." Nikamwendea mke wangu, nikasema, "Mpenzi, huenda huu ukawa ndio mwisho wangu. Sijui." Ni wangapi wamewahi kuisikiliza hiyo kanda? Vema, hakika, mnajua. Mnaona? Nikasema, "Ni BWANA ASEMA HIVI. Jambo fulani liko karibu kutukia, sijui." Ndipo basi nikamwendea, na nikasema, "Mpenzi, nitakwambia kile ambacho ninataka ufanye sasa. Ikiwa huu ndio mwisho wangu, Mungu ameonyesha ono."

112 Yeye si kila mara anakwambia kile kilicho. Kamwe hakuwaambia ma—manabii wa Agano la Kale, au Agano Jipya, kile kilichokuwa. Mara nyingi, isipokuwa Yeye alitaka wao wajue, waliandika tu chini, mnaona, kwa hiyo haikuwa shughuli yao. Ni Mungu akitenda jambo fulani.

113 Kama Mungu hakuwa amejitokeza jukwaani, dakika kumi na tano majuzi asubuhi kabla sijaondoka, kanisa hili lisingekuwako hapa ila muda kidogo zaidi. Mwulizeni Ndugu Carlson. Kama Bwana Mungu hakuwa amesema nami dakika kumi na tano kabla sijaja hapa, ningesema, katika Jina la Bwana, kanisa hili lisingekuwa limesimama miezi sita kuanzia sasa. Mngetawanyika kama kondoo. Lakini Bwana Mungu, katika rehema Zake, alisema nami, pasipo kujua hata jambo moja kulihusu, kisha nikaja nikamwambia Ndugu Carlson.

Mara ghafla pale likafunuliwa, na hilo hapo. Sasa huyu hapa Ndugu Carlson. Mnaona?

114 Loo, nina furaha sana kwamba, katika wakati wa shida, Yeye yumo chomboni. Amina.

115 Jinsi Jina la Bwana libarikiwe! Laiti ningalikuwa na maneno, ningalikuwa na msamiati, namna fulani ya neno ambalo ningeelezea kile Yeye anachomaanisha kwetu. Hata hivyo, halina neno. Sisi...Yeye, Yeye...Na—nabii alisema, "Yeye ni Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele," ndipo basi maneno yakamwishia, akasema, "Yeye ni wa ajabu." Hakuwa na vyeo vingine zaidi angaliweza kumpa Yeye. "Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele, na wa Ajabu." Amina. Loo, jinsi tunavyomsifu huyo Bwana Mungu Yehova mwenye nguvu, aliye mkuu!

116 Katikati ya uabudu sanamu, katikati ya itikadi za ulimwengu, katikati ya namna zote za machafuko na kuchanganyikiwa, tungali na Yeye kwenye chombo. Loo, katika siku hii, katika siku hii ambapo dini hazijui zielekee njia gani; loo, jinsi nilivyo na furaha kujua ya kwamba Mungu yuyo huyo, pamoja na Utukufu ule ule wa Shekina, yeye yule jana, leo, na hata milele, yumo chomboni, nikijua sina budi kukabiliana (kama Yeye akikawia) na bonde la kivuli cha mauti. Si ajabu Daudi alipaza sauti, "Sitaogopa uovu wowote, kwa kuwa Wewe umo chomboni!" Amina.

117 Loo, jinsi ambavyo wangeweza kuona jambo hili, mengi sana waliyokuwa wameona, hawakuweza kuelezea yote, ya yale waliyokuwa wameona. Sasa iliwafunukia ya kwamba Yeye alikuwa amelala papo hapo karibu nao.

118 Sasa Yeye yuko karibu zaidi na wewe kuliko alivyokuwa wakati huo. Hiyo ni kweli? "Niko pamoja nanyi sasa, bali nitakuwa ndani yenu. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, hata hivyo nyinyi mtaniona Mimi; kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho wa ulimwengu."

119 "Ndugu Branham, ninaweza kuhakikishiwa jambo Hili?" Yesu alisema hivyo! "Nitajuaje hilo?"

120 "Na kazi nizifanyazo ninyi pia mtazifanya." Haya basi. Je! mnaliamini? Vema, "Yeye yule jana, leo, na hata milele!"

121 Nafikiri wakati umewadia, wakati shida zinapoingia, hata tunasema, kwa wale wanafunzi ambao hapana shaka walisema, "Twendeni tukamwamshe. Twendeni tukamwite. Na tumwite Yeye jukwaani." Loo, ndugu yangu mpendwa, dada yangu mpendwa, ninawapenda. Basi, kumbukeni, ninawaambieni Ukweli. Kama una shida usiku wa leo, Yeye yuko karibu kabisa. Anaweza kuitwa jukwaani, kwa msogeo tu wa midomo yako. Yeye atakuja jukwaani. Amina. Mwiteni Yesu jukwaani!

Mwamsheni Yesu, kwa kuwa tunaye pamoja nasi, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

122 Walikuwa wameliona Neno la Mungu la Kimaandiko likithibitishwa na Yeye, na sisi pia tumeona, na Yeye hakuwa mgumu kuitwa jukwaani. Alikuwa tu amelala pale akiwangojea wamwite Yeye.

123 Sasa nashangaa, usiku wa leo, kama Yeye halali tu moja kwa moja moyoni mwako, akikungojea umwamshe? Hiyo ni kweli. Loo, ninapenda hilo!

124 Watu leo hii wanasema, "Vema, sasa, laiti tungalijua tu na kuhakikishiwa." Tunawasikia wakisema, wakisema, "*Hili* ni *lile*, na *hili* ni *lile*."

125 Lakini *Hili* ni Lile. *Hili* ni Lile. Sasa, *Hili* ndilo Yeye alilosema, Hili ni Neno Lake. Yeye na Neno Lake ni kitu kile kile. Acha Neno Lake limtambulishe Yeye.

126 Hivyo ndivyo vile Yeye alisema ingethibitisha Yeye alikuwa ni Mungu, kwa sababu kwamba kazi ambazo Mungu alimpa Yeye kufanya zilifanywa na Yeye. "Kama sizifanyi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi." Mnaona? Hivyo ndivyo ilivyomtambulisha Yeye.

127 Hiyo ndiyo njia ya kukutambulisha wewe. Ukisema wewe ni Mkristo, na u—utambulisho wa Mkristo, Mkristo wa Biblia, haujafanyizwa ndani yako, basi kuna kasoro fulani. Mnaona, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Naam, bwana. Si "labda zitafuatana nao." Zitafuatana!

128 Laiti tungaliweza tu kutambua ya kwamba Yeye yupo hapa pamoja nasi, yeye yule jana, leo, na hata milele. "Lo, niko pamoja nanyi sikuzote. Sitawaacha kamwe, sitawapungukia. Niko pamoja nanyi hata mwisho wa ulimwengu," Mlango wa 24. "Sitawaacha kamwe," tena Yeye alisema. Loo! Tena, "Sitawaacha kamwe wala kuwapungukia." Nilikuwa tu nikiyaangalia Maandiko niliyokuwa nimeandika hapa kuhusu hilo.

129 Tunawezaje kuwa na hakika? Kwa Neno Lake lililothibitishwa. Yeye sasa anawangojea kumwita jukwaani, kuthibitishwa, kwa hiyo hebu twende tukamwamshe Kristo katika maisha yetu.

130 Unamwamshaje Kristo? Kwa kuliamini Neno Lake. Imani humleta Yeye jukwaani. Hiyo ndiyo humleta Yeye jukwaani, imani. Basi, mwiteni Yeye akalithibitishe Neno Lake. Wala msitie shaka, katika hofu; msifanye hivyo. Mwamini tu kama Hilo lilivyoandikwa, na hebu litendeke, naye Mungu atawathibitishia ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele.

Tunamwabudu Mungu asiyeonekana.

131 Kama mtu akija juu ya jukwaa hili, usiku wa leo, akiwa na makovu ya misumari mikononi mwake, na alama za miiba kote hapa, huyo asingekuwa ni Mungu. Tumekuwa na mengi sana ya hayo katika siku za mwisho. Mnaona? Vema, mnafiki yeyote angeweza kufanya hivyo. Mnaona, mwigaji yeyote, tapeli, angeweza kufanya hivyo. Lakini njia pekee ungaliweza kumjua Yesu ilikuwa ni kwa kazi Zake. Na mtu huyo angekuwa akijaribu kujifanya mwenyewe Yesu; na Yesu hataonekana katika mwili wa nama hiyo mpaka tutakapomwona Yeye Akija. "Kutakuwako na makristo wa uongo watakaoinuka katika siku za mwisho," Yeye alisema, "na wataonyesha maajabu makuu, ishara kuu," bali hilo lingali silo.

132 "Kwa kuwa kama kimulimuli cha radi kinavyotoka Mashariki, na kinamulika hadi Magharibi, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu."

133 Lakini tunajuaje basi ya kwamba Yeye yuko pamoja nasi, katika ninii. . . katika umbo gani? Sio kwa mawazo ya kiakili; hayathibitishi katika maisha yao. Sio kwa kusema, "Ninaamini." Hilo halilifanyi. Inapaswa kuwa ni jambo fulani likitukia ndani yako, ambalo, Roho Mtakatifu Mwenyewe, huyo ndiye thibitisho la Mungu.

134 Na kama ukisema unaye Roho Mtakatifu, na halafu usiamini kila Neno humu ndani, kuna kasoro fulani na roho uliyo nayo. Roho Mtakatifu aliandika Biblia, na Yeye hawezi kusema, "Nilidanganya *pale*. Sikumaanisha *Hilo*." Si Yeye; Yeye ni mkamilifu.

135 Angalia, Yeye anatambulishwaje, Yeye angeweza kitu gani? Kama Biblia ilisema, Wakolosai 1:15, ya kwamba sisi—sisi ni. . . tunamwabudu "Mungu asiyeonekana." Mungu ni asiyeonekana. Mnaamini hilo? Basi mtu huyu anayejitokeza hapa na makovu ya misumari, na moshi, na damu, na kila kitu kingine, hilo lisingemfanya kuwa ni Mungu. Tunamwabudu Mungu asiyeonekana. Yeye daima amekuwa asiyeonekana mpaka alipojitambulisha Mwenyewe ndani ya Yesu Kristo. Je! hiyo ni kweli?

136 Sasa Mungu asiyeonekana anajitambulisha Mwenyewe ndani yako. Mnaona? Wewe ni hekalu Lake. Nyinyi ni ninii. . . "Mwili wako ni hekalu la Roho Mtakatifu." Maandiko yanasema hivyo.

137 Nguzo ya Moto ambayo Musa aliiona haikuwa ndiyo Mungu asiyeonekana. Hiyo Nguzo ya Moto ilikuwa ni Utukufu wa Shekina uliowakilisha ya kwamba Mungu asiyeonekana alikuwa karibu.

138 Wakati Yohana alipombatiza Yesu, Mwana wa Mungu; Mungu, Mungu asiyeonekana, alishuka katika umbo la Nuru, akiwa na umbo kama hua akishuka chini kupitia hewani, Mungu asiyeonekana akitambulishwa katika Utukufu wa Shekina.

139 Mungu yeye yule asiyeonekana akijitambulisha Mwenyewe katika Nguzo ya Moto, Utukufu wa Shekina, wakati walipoliweka wakfu hekalu wakati wa Sulemani. Iliingia na ikaenda . . . Nguzo ya Moto iliingia nyuma ya mapazia, juu ya Patakatifu pa patakatifu. Utukufu wa Shekina ulitambulishwa.

140 Sasa, wakati Paulo alipokuwa akienda zake Dameski, Yesu Kristo asiyeonekana alijitambulisha Mwenyewe kwa Paulo, katika umbo la Utukufu wa Shekina, Nuru iliyoyapofusha macho ya huyo mwenye dhambi. Amina.

141 Utukufu uo huo wa Shekina upo hapa usiku wa leo, yeye yule jana, leo, na hata milele, akiwakilisha Mungu asiyeonekana, akithibitisha Neno Lake kwa ishara zile zile Yeye alizoahidi kufanywa. Yeye ameshaitwa jukwaani.

142 Sasa waweza kumwita Yeye maishani mwako, na kusema, "Bwana Yesu, ninamchukua Yeye, ninakuchukua Wewe kwenye Neno Lako. Ninaamni ya kwamba Wewe upo hapa. Ninaamni ya kwamba Wewe upo hapa, usiku wa leo, kunisaidia. Ninakutaka Wewe chomboni mwangu. Ninakutaka Wewe, Roho Mtakatifu mkuu, uje kwangu. Niko taabuni. Mimi ni mgonjwa. Mimi ni mwenye dhambi. Ni—ninataka Wewe unijie, nataka Wewe unisaidie. Ninatambua ya kwamba Wewe umekaa pale tu, ukingojea kuninii, mimi kukuita Wewe. Nami ninaenda kukuita Wewe, kwa moyo wangu wote"?

143 Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu tunapofanya hivyo. Iweni na kicho. Ombeni kama ambavyo hamjawahi kufanya hapo kabla.

144 Kila mtu atulie kwa dakika moja na kuwazia. U nani wewe? Wewe ni kitu gani? Ulitoka wapi, unaenda wapi? Kama ulikuwa mwenye dhambi hapa ndani usiku wa leo ambaye hamjui Kristo, na ungetaka Yeye aingie chomboni mwako usiku wa leo na kukusaidia kupitia kwenye maji yenye tufani, nawe unataka kukumbukwa katika maombi, waweza kuinua mkono wako? Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe, wewe, wewe, kote jengoni.

145 Hivi hutakumbuka tu sasa, ninapokuombea, ya kwamba utaufungua tu moyo wako. Hayo ndiyo yote kwake. Kiri tu, useme, "Bwana, nimekosea. Ninakutaka Wewe unikumbuke."

146 Bwana Mungu, umeiona mikono hiyo. Watu hao, ninaamini, Baba. Ni—ninasimama hapa kati ya Uzima na mauti, kwa ajili yao. Nami ninatambua, kwenye Siku ya Hukumu, ninaenda kuwajibika kwa ajili ya yale ninayofanya sasa hivi. Nami ninaomba, katika maombi, kwa ajili yao, Bwana, ya kwamba ule Utukufu mkuu wa Shekina wa Mungu utawatokea, saa hii. Haitawaacha kamwe maishani mwao mwote. Na kote kupitia maishani, katika kila shida ndogo, jalia Utukufu huo wa Shekina uwepo, wajue Huo unaweza kuitwa jukwaani wakati wowote.

147 Walisema katika Maandiko, Baba, ya kwamba, "Walikuchukua Wewe, jinsi Wewe ulivyokuwa, na kukuweka Wewe chomboni."

148 Bwana Yesu, Wewe ni Roho, usiku wa leo, hapa katika umbo na jina la Roho Mtakatifu. Ee Mungu, kwa imani tunakuchukua Wewe jinsi ulivyo, ndani ya chombo chetu, Baba. Tusaidie, Mungu. Acha Utukufu wa Shekina uonekane kwetu na utupe amani.

149 Sijui lolote lingine la kufanya, Bwana, ila kusema hili ambalo Wewe ulisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza, na wote ambao Baba amenipa Mimi watakuja Kwangu." Na kutoka nyuma ya mikono hii, ambayo ninaamini walikuwa waaminifu, ambao waliinua mikono yao Kwako. Ninaomba, Bwana Yesu, basi, kama mtumishi Wako, ninawatoa Kwako, kama tunu za mkutano huu hapa Chicago.

150 Nikimwamuru ibilisi asiwaguse tena! Hao ni mali ya Mungu. Ondoa mikono yako, Shetani, mpaka watakapokuwa imara kabisa na wajue jinsi ya kuenenda na kumpinga adui. Ninamwamuru adui, kupitia Yesu Kristo, akae mbali nao.

151 Jalia Roho Mtakatifu mpendwa awachukue, awaongoze kwenye ubatizo wa maji, na kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, kisha kuwatia muhuri katika Ufalme wa Mungu hadi Kuja na kuonekana kwa mwili usioonekana wa Bwana Yesu kumnyakua Bibi-arusi Wake. Hao ni Wako, Baba. Jalia Mungu mkuu wa Utukufu wa Shekina awe pamoja nao sasa na hata milele. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba. Amina.

152 Sasa hebu kidogo. Hilo ndilo jambo la kwanza kufanya. Sasa jambo la pili la kufanya, kama umemkubali Yeye, itakuwa ni kulishuhudia, kwa kuwa Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yako. Yeye hawezi kukusaidia mpaka kwanza, kwa imani, umkubali Yeye na—na ushuhudie hadharani ya kwamba Yeye ni Mwokozi wako. Yeye, kama utamshuhudia Yeye hapa... Utamwonea haya hapa, Yeye atakuonea haya Kule. Iwapo humwonei haya hapa, basi Yeye hatakuonea haya Kule. Nafikiri, wakati wa kufungwa mkutano huu, kwamba kila mmoja wa watu hawa uliyemkubali Kristo kama Mwokozi wako, unapaswa kuja kwenye jukwaa hili na kusema kile Mungu amefanya moyoni mwako.

153 Sasa, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, Yeye alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa."

154 Sasa hakuna kadi za maombi. Hao watu, tuliwaombea wagonjwa hivi majuzi usiku, bali ninajisikia kushurutishwa kufanya jambo hili. Ni wagonjwa wangapi walio humu ndani, inueni mikono yenu. Ninyi mlio wagonjwa na wahitaji. Mungu anajua nyinyi ni nani. Iweni tu na imani.

155 Sasa mtu yeyote asisogee, kutoka, kwa—kwa dakika chache zijazo. Hili ni jambo kubwa. Ni kubwa sana!

156 Kwa hiyo kukiweko na asiyeamini hapa ambaye haliamini, ninakupa changamoto, katika Jina la Yesu Kristo, kuja hapa na kulifanya. Kama unajua njia nyingine yoyote mbali na Neno la Mungu na—na kile hili lilicho, Neno la Mungu, ninataka kuliona likifanywa. Basi, kama huwezi, basi liamini.

157 Sasa hebu kila mtu humu ndani aangalie moja kwa moja huku; ama, aangalie juu, hilo ni bora zaidi. Ninahofia nitavutia usikivu wenu kwenye kitu ambacho sipaswi kuwavutia. Kama Petro, Yohana alivyosema, "Tuangalie sisi." Silimaanishi jinsi hiyo. Hebu, hebu tuangalie juu.

158 Nami nitanukuu Andiko jingine. "Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu," tunajua hilo, "na Yeye pia ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Hiyo ni kweli?

159 Sasa nitaangalia na kuona ni nani ninayemwona ambaye ninamjua, maana ninao watu fulani hapa, wanaoketi hapa, kutoka maskanini kule nyumbani. Na mmoja wao ndio kwanza nimtambue, ni, yeye huja kule chini, ni Bibi . . . Jina lake lilikuwa ni Griffin. Ninasahau jina lake sasa. Ni Dada Rosella hapa, yeye na mama yake wameketi hapa. Yule mlevi sugu wa Chikago, ndipo Bwana alimponya katika mkutano. Ninyi nyote, karibu, mnamfahamu Rosella hapa; ile misheni, na kadhalika, mahali alipoenda, akishuhudia. Mlevi sugu kabisa, na sasa Mkristo wa kupendeza, naye aliitwa tu na Utukufu ule ule wa Shekina. Unadumu, pia, sivyo, Rosella? [Dada Rosella anasema, "Amina."—Mh.]

160 Na sasa ninaangalia kote tena. Sina uhakika, bali nafikiri ninamfahamu mama huyu aliyeketi hapa, papa hapa, mwanamke wa pili papa hapa, aliyeweka mikono yake kinywani mwake. Siwezi kukumbuka jina lake. Naam, wewe. Si wewe huja huko maskanini? Ni Bibi Peckinpaugh? Hiyo ni kweli? Hivyo ndivyo nilifikiri lilikuwa. Vema.

161 Halafu kulia, mwanamke wa tatu nyuma, ni Bibi Way, mke wa mtu huyu aliyeanguka akafa kanisani hivi majuzi, kwa mshtuko wa moyo, naye akafufuliwa, ameketi hapa.

162 Kuna mtu aliyewahi kumwona mtu yeyote aliyefufuka kutoka kwa wafu? Kama hujawahi kuona, inueni mikono yenu, hamjawahi kumwona mtu yeyote aliyefufuka kutoka kwa wafu. Simama, Bw. Way.

163 Nilikuwa nikihubiri kama tu sasa, Utukufu wa Shekina ukiweko, na mara ghafla, katika mshtuko wa moyo, macho yake yakarudi nyuma. Sasa unaweza kufumba macho yako, bali huwezi kuyarudisha macho yako nyuma. Mke wake pale ni nesi aliyesajiliwa, wa miaka mingi, alipiga mayowe wakati aliposhika moyo wake na kuona ameenda. Nikatuliza kusanyiko, nikashuka chini. Nilikuwa nikizungumza. Nikaweka

mikono yangu juu yake, nikahisi. Nikaangalia juu kumwona, naye akasema, "Ametuacha." Nami nikayajaribu macho yake, nikaona macho yake huko... upande wa nyuma hapa, sehemu ya ngozi, ilirudi nyuma namna *hiyo*. Hakuwa na mapigo ya moyo zaidi ya *hiki* kilicho nayo.

164 Nikasema, "Bwana Yesu," ndipo Yeye akaja jukwaani.

165 Nikaweka mkono wangu juu yake. Naye akasema, akajaribu kuzungumza, "Ndugu Branham..." Alikuwa dhaifu sana hangeweza kuninii... Naye huyu hapa amesimama, usiku wa leo, tunu ya neema ya Mungu.

166 Sasa hivyo ni, angalau, visa vitano ama sita dhahiri vya kuwa mfu, wakati mwingine kwa saa sita ama nane, wamefufuliwa, kwa Uwepo wa Yesu Kristo, kupitia maombi.

167 Sina hakika sana, juu ya maskini mama anayeketi hapa, ninaamini ndiye. Ninakujua. Sijui jina lako ni nani, bali kukujua wewe. Kweli?

168 Halafu basi Ndugu Brown, ninaamini hiyo ni kweli, kama sijakosea, ameketi... Huyo ni Ndugu Brown? La, sidhani ndiye. Samahani. Vema, karibu ni hivyo tu, ninaamini.

169 Wewe omba sasa, useme, "Bwana Yesu, jalia niguse vazi Lako, Wewe ni Kuhani Mkuu. Na ni—ninajua ya kwamba Ndugu Branham, ya kwamba hanijui, hajui chochote kunihusu mimi. Lakini Wewe unanijua. Na kama utaniruhusu tu niguse vazi Lako. Na—nataka kuwa mzima." Sasa ninyi ombeni katika ombi hilo.

170 Nami ninamwomba Mungu jambo hili. Bwana Yesu, na katika kufunga mkutano huu usiku wa leo, ya kwamba watu hawa, labda ni wageni langoni, nao huenda wasielewe, bali hebu na wajue ya kwamba Ujumbe ni wa kweli. Njoo, Bwana Yesu, na utujalie sisi. Na jalia tujisalimishe wenyewe, pamoja, hata asiyeamini ama hawa Wakristo waliozaliwa upya waweze kuona kwamba Utukufu wa Shekina wa Mungu upo hapa sasa, umetambulishwa na picha, pia na sayansi, katika makanisa kote ulimwenguni. Wewe ni yule yule jana, leo, na hata milele. Tunakuamini Wewe.

171 Hebu Bwana Yesu... [Dada anaanza kunena kwa lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Bwana asifiwe. Sasa Mungu amejitambulisha Mwenyewe hapa. Sasa, ninaamini hiyo kuwa ni kweli.

172 Sasa hebu mtu fulani kupitia sehemu hizi *huku*, kisha tutaingia *hivi*, halafu kadhalika, huku. Nanyi aminini tu kwamba... Sasa mtu yeyote asisogee huku sasa. Iweni na kicho kabisa.

173 Sasa sisemi ya kwamba Yeye atalifanya. Ninatumaini Yeye atalifanya. Lakini kama atalifanya, hivi hilo halitakuwa thibitisho la Neno hili, kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na

hata milele? Hivyo ndivyo nyinyi watu mlivyojua Yeye alikuwa ni Masihi hapo mwanzo? Basi Yeye anajitambulisha Mwenyewe ndani ya kanisa Lake, usiku wa leo, ya kwamba Yeye ni Masihi yule yule, ikiwa tu utaamini.

174 Sasa ombeni tu. Sina budi kuweka wakfu njia moja . . . kuwa makini, hasa, njia moja, kuwaangalia tu watu na kuona. Mimi—mimi . . .

175 Naam, Mungu ashukuriwe, Hii hapa. Katika Jina la Yesu Kristo, ninachukua kila roho hapa ndani chini ya mamlaka yangu, kwa ajili ya Utukufu wa Mungu. Sasa mnajua kile hilo linachomaanisha. Iweni na kicho.

176 Ile Nuru inaning'inia juu ya maskini mwanamke anayeketi papa hapa nyuma, mwanamke kijana, aliyevaa nguo ya waridi. Anaomba kumhusu mume wake. Amerudi nyuma, ameketi pale nyuma kabisa karibu na nguzo. Yeye ataliamini, alikubali, na Mungu atafanya mwujiza huo kwa ajili yako kama utaamini.

177 Mama anayeketi karibu na wewe anashangaa juu ya mumewe . . . La, ni kaka yake ambaye anaenda kulazwa hospitalini, kesho, Hospitali ya Askari Wakongwe. Kama utaamini pia, itafanya kazi kwako, pia, kama unaweza kuliamini.

178 Huyu hapa mwanamume. Bwana akubariki. Likubali tu. Unaweza kupata ulichoomba.

179 Kuna mtu ambaye amefanyiwa upasuaji, kwa ajili ya kansa, ameketi hapa. Kama utaamini, Mungu atakupa afya. Unaamini? Bw. Wilcox, simama kwa miguu yako, kubali uponyaji wako. Baba wa Mbinguni anajua sijawahi kumwona mtu huyo, maishani mwangu. Hiyo ni kweli. Usiwe na wasiwasi, bwana. Sisi hatufahamiani; pungianeni mikono mmoja kwa mwingine. Hiyo ni kweli.

180 Ni kitu gani? Utukufu wa Shekina; Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.

181 Huyu mama mweusi hapa mwenye ngiri, matatizo. Bibi Burnet, unaamini ya kwamba Bwana Yesu atakupa afya? Basi waweza kuupokea. Amina. Sijawahi kumwona mwanamke huyo, maishani mwangu.

182 Kuna pumu, ameketi nyuma pale, akiugua, yule mtu anayeniangalia moja kwa moja. Loo, kama ninaweza kuwa . . . Bwana ataniambia ni nani . . . Bw. McGill, simama kwa miguu yako na uukubali uponyaji wako, katika Jina la Yesu Kristo. Sijawahi kumwona mtu huyo, maishani mwangu. Mungu Mwenyezi anajua.

183 Mwingine hapa. Huyu hapa mwanamume hapa, ana mvilio wa damu moja kwa moja karibu na moyo wake, ameketi kwenye safu ya nyuma huko. Unaamini ya kwamba Mungu Mwenyezi

atakuponya na kukupa afya? Ndilo tumaini pekee ulilo nalo, la kuishi.

184 Mwanaume huyu anayeketi papa hapa mwishoni, anamwombea mtu aliye huko Norwe, akimwombea rafiki yake. Mtu huyo mwenyewe anaugua ugonjwa wa mgongo. Hiyo ni kweli, sivyo? Inua mkono wako. Jambo ndilo hilo, umepata kile unachotaka.

185 Mwite Yeye! Yeye yupo hapa. Yuko ndani ya chombo. Mnamwamini Yeye?

186 Simameni kwa miguu yenu, basi, na mseme, “Bwana Yesu Kristo, nitakuita Wewe sasa. Ninakuamini Wewe. Ninakuita Wewe uje jukwaani, kwa ajili ya nafsi yangu.” Inua mkono wako, na kwa njia yako mwenyewe, taja haja yako kwa sauti kuu. Ni wewe. Wewe ndiwe uliye mgonjwa. Yeye Huyu hapa, amejitambulisha Mwenyewe kikamilifu, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Utukufu kwa Mungu!

Baba wa Mbinguni, saidia sasa hivi tu katika wakati huu wa uhitaji.

187 Ninampa Shetani changamoto, katika Uwepo wa Yesu Kristo aliyetambulishwa. Kwa ajili ya leso hizi, na kwa ajili ya watu hawa; Shetani, huwezi kuwashikilia. Yesu Kristo na akukemee! Watu hawa wanaamini ya kwamba Yeye yuko chomboni. Yeye yupo hapa sasa. Utukufu Wake wa Shekina uko juu yetu. Toka hapa, Shetani! Nakupa changamoto, katika Jina la Yesu!

63-0804E Kumwita Yesu Jukwaani
Marigold Center
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org